

Jiandae kupambana na maambukizi ya virus vyatya corona

Hatua 6 za kufuata kwa mtoha huduma za afya

Hivi ni aina mpya ya virus (**COVID-19**), ambavyo viligundulika kwa mara ya kwanza China December 2019, vikisababisha mlipuko wa homa kali ya mapafu kama vile (homa, kukohoa, na kushindwa kupumua).

Ni muhimu kila kituo cha huduma za afya kujenga utayari wa kupambana na maambukizi ya COVID-19 kwa kuchukua hatua zifuatazo:

1

Muhimu

- Wataarifu wagonjwa na watumishi wa afya mambo muhimu ya kujikinga na COVID-19.
- Sisitiza usafi wa mikono, Kupunguza maambukizi unapokohoa kukaa mbali na wengine na kujizuia kugusa macho, pua na mdomo.

2

Pata taarifa sahihi

- Pata taarifa sahihi za COVID-19 kila mara kutoka kwa mamlaka husika kwa mfano, kutoka wizara ya afya na Shirika la Afya Duniani (WHO). Yajue maeneo yalioathirika zaidi kwa maambukizi.
- Bandika vipeperushi vinavyoolezea COVID-19 kwenye mbao za matangazo na sehemu ambazo wagonjwa na wateja watazunga kwa urahisi.

3

Fundisha

- Tumia miongozo iliyotolewa na wizara ya afya au tengeneza muongozo wa dharura wa kituo wa namna ya kujikinga na kuthibiti maambukizi.
- Toa mafunzo kwa wotoa huduma za afya kituoni kwako kuhusu dalili za maambukizi na miongozo ya jinsi ya kukagua, kutambua na kutibu wagonjwa wa COVID-19.

4

Tenga wagonjwa wenye dalili

- Weka mtoha huduma kwenye sehemu ya kuingilia kituoni ili aweze kuuliza na kutambua wagonjwa na wageni wenye dalili. Wape wagonjwa wenye dalili tishu au viziba mdomo na pua kisha dhibiti idadi ya wasindikizaji au wageni ambaio sio wagonjwa.
- Watenge wagonjwa wenye dalili za maambukizi kwenye sehemu maalum iliyoandalisha na yenyehewa ya kutosha.
- Chukua vipimo na fuata taratibu za rufaa na kumsafirisha mgonjwa kadiri ya miongozo ya wizara au WHO.
- Hamasisha watoa huduma na wafanyakzi wengine ambaio ni wagonjwa kubakia majumbani mwao.
- Ikiwa kuna mshukiwa wa COVID-19 kwenye kituo chako usihamanike bali toa taarifa kwa kiongozi wako kazini au piga simu iliyoandikwa hapo chini.

5

Tumia mbinu za kulingia na kudhibiti maambukizi na vifaa kinga binafsi

- Gawa vifaa kama tishu na sabuni katika sehemu ya kunawa mikono na vitakasa mikono vyenye asilimia 60%-95% ya spiriti.
- Weka chombo cha kutupia tishu chenye mfunikoo karibu na sehemu ya kunawia mikono.
- Hakikisha matumizi sahihi ya vifaa kinga binafsi endapo kuna mgonjwa mwenye dalili.
- Takasa kituo chako na safisha vitu na maeneo ambayo yanaguswa mara kwa mara.

6

Hakikisha una mahitaji muhimu ya kutosha

- Hakikisha kuna vifaa kinga binafsi vya kutosha.
- Hakikisha kuna mahitaji mengine ya kutosha kama vile maji, sabuni, vitakasa mikono na tishu.

Ikiwa unashuku kuna mgonjwa mwenye maambukizi piga namba iliyoandikwa hapo chini:

 Mapendekazo haya yanaendana na miongozo ya Shirika La Afya Duniani (WHO). Taarifa hii imenza kutumika rasmi kuanzia tarehe 26-Machi 2020. Mwongozo wa matibabu COVID-19 hubadilika mara kwa mara. Pata taarifa sahihi kwa kuwasiliana na mamlaka husika na pia tembelea tovuti ya Shirika la Afya Duniani kuitia www.who.int.